Mothers' UNION



# Shajara ya Maombi 2022

Kuunganisha wanachama kwa sala
na ibada duniani kote

4 **Barua ya Raisi wa duniani kote:** Sheran atambulisha Shajara ya Maombi ya 2022

5 **Maombi ya Pamoja:** kuelezea Wimbi la Maombi

42-43 **Ramani ya Uanachama:** Mahali tulipo ulimwenguni

## IMANI KWA VITENDO

*Jinsi ambazo Ushirika wa Akina Mama unaleta matokeo chanya katika ulimwengu wetu*

8 Maeneo salama kwa walionusurika Sudan Kusini

13 Kuondoa umaskini nchini Burundi

20 Msaada kwa waliotengwa nchini Rwanda

30 Kutafuta uponyaji kwa waadhirika wa kiwewe nchini msumbiji

41 Kupambana na unyanyasaji dhidi ya wanawake katika mikoa

53 Kuhimiza uwezeshaji na usawa nchini DRC


74 Kuleta matumaini kwa walio gerezani

79 Kusimama kupinga Unyanyasaji wa Kijinsia









## SHAJARA YA MAOMBI

*Kila mwezi katika shajara huanza na tafakari, maombi ya ufunguzi na shughuli ya maombi ya ubunifu unayoweza kutumia kama nyenzo.*


6 **Januari:** Wakati wa mabadiliko

14 **Februari:** Kujitegemea

21 **Machi:** Kuthamini wanawake

28 **Aprilii:** Sadaka na ufufuko

35 **Amani: na usalama**

44 **Juni:** Roho, kanisa na ufalme

51 **Julai:** Familia na mahusiano

58 **Agosti:** Maono na Utume wa Ushirika wa Akina Mama (UAM)

65 **Septemba:** Wimbi la Uumbaji

72 **Oktoba:** Masuala ya kijamii

80 **Novemba:** Haki ya kijinsia

87 **Desemba:** Majilio na Krismasi












*The Prayer Diary* (Shajara ya Maombi) ni rasilimali ya kuongeza maarifa kwa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama, inayochapishwa mara moja kwa mwaka na kusambazwa kama sehemu ya usajili wa kila mwaka, kwa wanachama na marafiki walio Uingereza na Irelandi. Wanachama wa nchi za kigeni na marafiki wanaweza kupokea nakala ya PDF kupitia barua-pepe kutoka mikoa ya ndani au kwenye mtandao www.mothersunion.org. *The Prayer Diary* imetafsiriwa kwa lugha za Kifaransa, Kihispania cha Amerika Kusini na Kiswahili

Kwa mawasiliano
Mothers' Union, Mary Sumner House,
24 Tufton Street, London, SW1P 3RB
T: 020 7222 5533
E: publications@mothersunion.org

www.mothersunion.org

**Namba ya usujili:** 240531

**Rais wa duniani kote:** Sheran Harper
**Mkurugenzi mkuu:** Bev Jullien

*The Prayer Diary* imechapwa na Mothers' Union

**Mhariri:** Adam Sach
**Mbunifui:** Arca Creative
**Kimechapwa na:** Halcyon Print Management Ltd

Karatasi iliyotumika katika chapisho hili imetengenezwa kwa kutumia mbao kutoka misitu endelevu na isiyo na klorini.

Huku kila juhudi ikiwa imechukuliwa ili kuhakikisha usahihi wa tarehe na maoni, Ushirika wa Akina Mama hauwezi kukubali jukumu kwa hasara yoyote, uharibifu au usumbufu unaosababishwa kwa makosa yoyote au upungufu.


© hati miliki ya yaliyomo 2021

# *Wapendwa,*



Shajara Yetu ya Maombi inaendelea kuwa chemchemi ya faraja na nguvu, inayowaunganisha watu wa tamaduni zote katika matendo ya kila siku ya sala, ibada na ushirika. Ni sehemu muhimu sana ya maisha yetu ambapo timu ya Mary Sumner House ilisisitiza kuiboresha kwa mara nyingine tena katika mwaka wa 2022, ili kukupa tafakari za kila mwezi na mawazo ya ubunifu ya maombi, ambayo yametoka mioyoni mwa washiriki wetu kote ulimwenguni.

Tunapopitia kurasa kila siku, naomba tuhamasike kutazamia siku zijazo tukiwa na maono mapya, tukiongozwa na mada yetu ya 2022: MABADILIKO - SASA! Mabadiliko haya huanza na neema ya Mungu, inayofanya kazi kwa nguvu ndani yetu, ikitufanya tufahamu mahitaji ya wengine na kutulazimisha kubariki maisha ya watu tunapoishi kwa imani yetu.

Safari yetu katika utatu mpya ijazwe na upendo wa Mungu, ambayo haijui mipaka – aina ya upendo unaobadilisha makanisa na jumuiya tunamoishi, unaoakisi ufalme wa Mungu na kuufanya Ushirika wa Akina Mama kuwa muhimu kwa maisha katika karne ya 21.

Naye akaniambia, “Neema yangu yakutosha. ...”
*2 Wakorinthho 12:9 (NKJV)*

Asante kwa upendo wako na kujitolea kwa Ushirika wa Akina Mama.
Kwa upendo na maombi yangu,

*Sheran*

Rais wa duniani kote

# Maombi ya Pamoja

**Kila siku saa sita mchana, washiriki wa Ushirika wa Akina Mama duniani kote huchukua mda ili kuomba. Tunamkaribia Mungu kwa uhakika, tukijua kwamba Mungu hutusikia na kuthamini maombi yetu.**

Kwa mwaka mzima, Wimbi la Maombi la kimataifa linaonyesha ahadi yetu katika maombi kwa ajiliya kila mmoja wetu, katika maeneo yote tunayofanyia kazi na kuishi. Tunazingatia maono ya siku zijazo ambapo kila mtu anaweza kustawi. Kwa kujiunga na kudumisha Wimbi hili la Maombi, tunaweza kuwa sehemu ya kitu kikubwa kuliko sisi wenyewe. Tunaposali, tunajua kwamba sisi pia tunaombewa na wengine ulimwenguni kote. Tafsiri za Shajara ya Maombi kwa lugha za Kifaransa, Kihispania na Kiswahili zinaendelea kutusaidia katika jitihada zetu za kufanya hivi.

Maombi haya ya kila siku yanaweza kutumika kujiunga na Wimbi hili la Maombi, kuombea kila jimbo kwa zamu. Kalenda imegawanywa katika sehemu za siku tatu, ikilenga kundi la majimbo. Katika siku moja ya juma kuna mstari wa Biblia wa kusaidia tafakari zetu, wakati tunaweza kuomba kwa ajili ya vipengele vya kazi yetu ambavyo hasa tunavifikiria.

Mungu utupendaye, tuite kuwa na huruma mpya kwa wengine, tunapofanya kazi ya kubadilisha maisha na jumuiya kote ulimwenguni. Tunakuomba utupe ujasiri wa kustahimili vurugu na dhuluma, kuchukua jukumu letu katika kuondoa umaskini. Hatuwezi kufanya hili peke yetu - tunahitaji kusimama pamoja, kushiriki nguvu na ujuzi wetu, tukiongozwa na Roho wako kuunda ulimwengu bora.

Bwana Yesu, utupe tunachohitaji ili kufuata wito wako juu ya maisha yetu kama wanafunzi wako, ili tuweze kuakisi neema na huruma yako kwa wote, kupitia kazi ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote. Leo tunaombea *

*tazama shajara ya Wimbi la Maombi.

> Sikuzote twamshukuru Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, tunapowaombea ninyi, kwa maana tumesikia juu ya imani yenu katika Kristo Yesu na upendo mlio nao kwa watu wote wa Mungu…
>
> Wakolosai 1:3-4

Na wajue kwa undani zaidi na kwa hakika upendo na neema ya Mungu inayowazunguka, kuwatia nguvu, kuwaongoza na kuwafariji. Mungu wa matumaini, Mungu wa amani, Mungu wa furaha, awepo kila wakati katika maisha yao kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Amina



# JANUARI: Wakati wa Mabadiliko



## Tafakari

'Kwake Mungu, yote yanawezekana': ni ahadi ya ajabu iliyoje na toleo la tumaini ambalo Yesu anatupa kwa mwaka ujao. Miaka miwili iliyopita imekuwa migumu na yenye changamoto, na jibu la kawaida limekuwa kukata tamaa, kujitosheleza na hata kujiondoa. Mwaka huu unaokuja, wenye muhula unaotarajiwa kuwa na ahueni, unatupa fursa nzuri ya kumwomba Mungu atusaidie kubadilisha maisha yetu. Kubadilisha tulivyo; kubadilisha jinsi tunavyotenda na jinsi tunavyoweza kuwahudumia vyema wale walio na uhitaji mkubwa zaidi, na kubadilisha jinsi tunavyoitikia uwepo wa Yesu pamoja nasi.

## Ombi la Kila Mwezi

Bwana mwenye upendo, badilisha maisha yetu ili tuweze kuangazia utukufu wa Kristo. Endeleza ndani yetu kazi ya Roho wako; muujiza wa mabadiliko ili kuakisi utukufu wa Kristo na kushiriki upendo wake ulimwenguni. Amina



## Ombi la ubunifu

Tafuta na ulinganishe picha mbili - moja nyeusi na nyeupe, na moja ya rangi. Zitafakari kwa muda, kisha uzitumie kama msukumo kuomba Mungu alete rangi katika maisha yetu ya kiroho, (kubadilisha) hali tunazokabiliana nazo na hali za wengine. Iwapo una karatasi ya kupaka rangi, tumia rangi tofauti ili kufanya mistari ionekane.Omba wakati unavyofanya hivi kisha utoe picha yako kama ombi la mabadiliko.

## Wewe, Bwana, wasikia haja ya walioteswa; unawatia moyo, na kusikiliza kilio chao...

*Zaburi 10:17 (NIV)*

Katika Dayosisi za Juba na Rejaf, Ushirika wa Akina Mama unafanya kazi ya kutekeleza Mpango wa Mafunzo ya Kusoma, Kuandika na Jinsia. MU inapanga kutambua na kuajiri wakufunzi wenye uzoefu ili kuwafunza Mabingwa wa Kujitolea wa Kusoma, Kuandika na Jinsia (VLGCs) kutoka kwa jumuiya katika dayosisi hizi mbili. Wakifanya kazi katika maeneo yao, kila VLGC itatoa mfululizo wa vipindi vya mafunzo kwa watu wazima katika kusoma na kuandika na mambo ya kijinsia kupitia vikundi rika vya kijamii. Inadhaniwa kuwa angalau 70% ya washiriki hawa ni waathirika wa Ukatili wa Kijinsia (GBV). Kwa kuwapa ujuzi wa kusoma na kuandika, MU itawezesha maeneo salama ambapo wanaweza kuzungumza kwa uwazi kuhusu yale waliopitia na kuanza mchakato wa uponyaji unaohitajika sana.

Kupitia elimu yao, washiriki watakuwa wachochezi wakuu wa maendeleo ya jamii, huku Sudan Kusini ikiingia kwenye demokrasia. Washiriki na wakufunzi wako katika nafasi nzuri zaidi ya kuangazia hatari za UWAKI. Watabaki katika jamii zao, ili kujenga kundi la watu walioelimika na kuhamasishwa ili wengine wanufaike.

*Juba, Sudan Kusini*



**Ombea:** walionusurika na UWAKI na mustakabali wa Sudan Kusini katika wakati wa mpito

---

## Wakati wa mabadiliko

JANUARI 1

### Jumamosi 1

Bwana mwenye upendo, badilisha maisha yetu ili tuweze kuangazia utukufu wa Kristo. Amina

**Wimbi la Maombi**

**Januari 1-3:** Wadhamini na wafanyakazi wa MU duniani kote

**Jumapili 2**
Asante, Bwana, kwa wale wote ambao wamekuwa tayari kusonga mbele katika majukumu ya Ushirika wa Akina Mama kwa miaka mitatu ijayo. Tafadhali wabariki, waandae, waimarishe na watie moyo katika yote wanayofanya katika huduma yako.

**Jumatatu 3**
Tunapotafakari kwa sala kuhusu vikundi vyetu vya ndani vya Ushirika wa Akina Mama, katika parokia na majimbo, tunakuomba wewe Roho Mtakatifu, uelekeze mwelekeo wetu na shughuli zetu, ili tufuate muongozo wako kwa kila njia.

**Jumanne 4**
Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha na amani yote mnapomtumaini, mpate kujawa na matumaini katika nguvu za Roho Mtakatifu. Warumi 15:13

**Jumatano 5**
Asante, Bwana, kwa wale wote ambao wametutia moyo na kutufundisha katika maisha yetu, hasa kama sehemu ya Ushirika wa Akina Mama. Tunapotazama nyuma kwa shukrani, tafadhali tuonyeshe jinsi ya kwenda mbele kwa imani - kusaidiana na kutia moyo kwa zamu wenyewe kwa wenyewe.

**Alhamisi 6** Epifania
Tunapotafakari leo kuhusu zawadi ambazo Mamajusi walimletea Kristo mchanga, ndivyo pia tunamletea vipawa na vipaji vyetu ili vitumike kwa utukufu wake, kupitia huduma yetu kama Ushirika wa Akina Mama ulimwenguni kote.

**Ijumaa 7**
Bwana Mpendwa, tafadhali tuonyeshe fursa unazotaka tuchukue, na watu unaotaka tuwatunze na kuwatumikia mwaka huu. Utupe ujasiri wa kufuata njia zozote mpya utakazotufunulia, ukijua kuwa utakuwa nasi katika yote.

**Jumamosi 8**
Leo tunatua kidogo ili kuwaombea wale tunaowajua wanaoumia au kuogopa.Tunaomba kwamba Mwaka Mpya uwaletee faraja, kitulizo, uponyaji na tumaini jipya, na sisi tutekeleze jukumu letu katika kufanikisha jambo hili. Bwana, kwa rehema zako - usikie maombi yetu..

### Wimbi la Maombi

**Januari 1-3:** Wathamini na wafanya kazi wote wa Ushirika wa Akina Mama duniani kote

**Januari 5-7:** Eswatini, Ruaha-Tanzania, Aguata & Lagos-Nijeria, Norwich-Uingereza, na Chotanagpur-India

**Januari 8-10:** Lesotho, Kibungo-Rwanda, Etche & Ogbomoso-Nijeria, Leeds-Uingereza na Hanuato- Visiwa vya Solomon

**Jumapili 9**
Kama vile kiwavi anavyokuwa kipepeo, mwenye umbo, sehemu, namna tofauti kabisa ya usafiri, chakula, rangi na mifumo, ndivyo tunavyoomba kugeuzwa kuwa yote Mungu anayotaka tuwe, tunapoona kazi yake maishani mwetu.

**Jumatatu 10**
Bwana unipendaye, nisamehe ninapoendelea kutambaa kama kiwavi, nikijifungia ndani ya mahangaiko yangu, badala ya kuangalia juu na kutoka nje, na kukufuata kwa uhuru kama kipepeo!

**Jumanne 11**
Tunabadilishwa tufanane naye kwa utukufu unaoongezeka daima, kutoka kwa Bwana, ambaye ni Roho. *2 Wakorintho 3:18*. Bwana, tusaidie tukuaangalie wewe leo, ili tuweze kutafakari upendo wako.

**Jumatano 12**
Tunakushukuru, Bwana, kwamba tuligeuzwa kuwa kiumbe kipya tulipoweka imani yetu kwako kwa mara ya kwanza. Tunaomba leo kwamba wengine wengi wapate upya wa maisha na furaha inayoletwa na hayo, wanapokumbatia maajabu ya upendo wako.

**Alhamisi 13**
Tunaomba tupate mabadiliko katika maisha yetu na familia zetu, katika jumuiya zetu na katika ulimwengu, kutoka gizani hadi kwenye nuru - kutoka huzuni hadi furaha. Tunaomba hasa kwa ajili ya mipango mingi ya MU ambayo inasaidia kuleta mabadiliko mema.

**Ijumaa 14**
Tunapoanza kuibuka kutoka katika janga la ulimwengu, tunaomba kwamba Mungu atubadilishe kibinafsi na kiroho na kutupa maono mapya ya siku zijazo. Na abadilishe MU, na makanisa na jumuiya ambazo sisi ni sehemu yake.

**Jumamosi 15**
Mabadiliko mara nyingi huhusu zaidi kutojifunza kuliko kujifunza. *Richard Rohr,* mwandishi wa Kikristo wa Marekani. Bwana tufungue roho zetu ili tuwe tayari kubadili mioyo na mitazamo yetu, ili tuwe zaidi kama Yesu na kutumikia ulimwengu katika jina lake.Jesús y sirvamos al mundo en su nombre.

**Wimbi la Maombi**

**Januari 8-10: Lesotho; Kibungo - Rwanda; Etche & Ogbomoso - Nijeria; Leeds- Uingereza na Hanuato-Visiwa vya Solomon**

**Januari 12-14:** Mauritius; Kericho-Kenya; Katsina-Nijeria; Kumasi-Ghana; Winchester – Uingereza na Nandyal - India

**Januari 15-17:** Shelisheli; Bukedi-Uganda; Enugu-Nijeria; Birmingham- Uingereza na Marathwada-India

### Jumapili 16
Baba, tunakushukuru kwamba leo Wakristo kote ulimwenguni wameungana kukuabudu wewe kama Mwokozi na Bwana. Ibada yetu iwe shahidi wa umoja wetu katika Kristo; sifa zetu na ziunganishwe kama sadaka yenye harufu nzuri, inayopanda juu mbinguni.

### Jumatatu 17
Mada ya juma la mwaka huu la maombi kwa ajili ya Umoja wa Kikristo ni "Tuliiona nyota yake mashariki na tumekuja kumwabudu." Bwana, unganisha kanisa lako na utuvute pamoja kwa nuru ya uwepo wako. Basi na sisi pia tuwe wachukuaji wa nuru yako, tunaposhuhudia kama kitu kimoja katika ulimwengu.

### Jumanne 18
Pendani kila mmoja. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mnapaswa kupendana. Upendo wenu ninyi kwa ninyi utauthibitishia ulimwengu kwamba ninyi ni wanafunzi wangu. *Yohana 13:34-35 (NLT)*

### Jumatano 19
Asante, Bwana, kwamba kama kanisa linavyoonyesha upendo, tunaweza kugeuzwa kuwa mwili mmoja unaoonyesha njia tofauti na ya kuvutia ya kuishi, njia inayoelekeza kwa Kristo.

### Alhamisi 20
Tunamshukuru Mungu kwa utajiri tulio nao katika mila zetu tofauti za Kikristo. Tunaomba tuwe wazi kukumbatia maonyesho ya imani ya kila mmoja wetu; tayari kumwona Mungu kwa njia mpya pamoja.

### Ijumaa 21
Kama watu wa Mungu, tunaweza kutimiza mengi zaidi pamoja kuliko kwa kujitenga. Bwana, tafadhali ondoa kingo zetu mbaya ili tuwe na umoja zaidi katika kuujenga ufalme wa mbinguni.

### Jumamosi 22
Omba leo kwa ajili ya mahusiano mazuri kati ya makanisa mbalimbali katika eneo lako. Mwombe Mungu nafasi za kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya jamii; ili umoja wenu uwe shahidi kwa ulimwengu uliovunjika.

### Wimbi la Maombi

**15-17 January:** Seychelles; Bukedi - Uganda; Enugu -Nijeria; Birmingham - Uingereza na Marathwada- India

**19-21 January:** St Mark the Evangelist - Afrika Kusini; Butare - Rwanda; Okigwe-South - Nijeria; Gambia; British Columbia - Kanada na Rajasthan - India

**22-24 January: Egypt;** Gasabo - Rwanda; Otukpo & On the Coast - Nijeria; Bathurst - Australia na Nasik - India

## Jumapili 23
Bwana ututie moyo wa kuonyesha upendo wako kwa wote wanaokuhitaji. Utuwezeshe kuwa sauti gizani, na uziongoze hatua zetu. Ututume kwa neema na amani yako ili tuwepo kwa ajili ya wale wanaotuhitaji, popote tulipo duniani. Amina

## Jumatatu 24
Tufikie mioyoni mwetu kwa matumaini na ujasiri, ili tuweze kupokea mabadiliko magumu, kufanya mabadiliko ya kweli na ya kudumu, kutafuta majibu mazuri halisi; kwa ajili ya familia na jumuiya zetu, nchi zetu na mabara yetu, watu wetu na sayari yetu, kwa ajili ya nafsi zetu wenyewe.

## Jumanne 25
Tazama nafanya mambo yote kuwa mapya - Bwana utuweke tayari kufanya kazi yako yoyote ambayo inaonekana kuwa mpya na ya kutisha kwa njia zetu za kisasa. Badilisha maisha yetu na utupe ujasiri wa Mary Sumner tunapoelekea katika siku zijazo.

## Jumatano 26,
Tazama, Ninafanya mambo yote kuwa mapya - Bwana badilisha maisha yetu hivi kwamba tuwe macho na tayari kukuona ukifanya kazi katika jumuiya zetu. Tupe dira ya malengo katika Ushirika wa Akina Mama popote pale tulipo duniani.

## Alhamisi 27
Sasa ni wakati unaokubalika - Bwana tusaidie kufahamu kwamba inatupasa kuamka na kuona kwamba kuahirisha hadi kesho si sehemu ya mpango wako wa Ushirika wa Akina Mama duniani kote.

## Ijumaa 28
Yesu, ulikuja kuleta utimilifu wa uzima kwa wote. Tusaidie katika miradi yetu yote ya mitaani na ya ulimwenguni, ili upendo wako unaoleta mabadiliko uonekane kwa wote.

## Jumamosi 29
Bwana wa nyakati zote, ukitimiza kusudi lako kwa manufaa ya wanadamu milele, utupe ufahamu,tuliozaliwa na imani kwako, ili tuweze kuishi katika uwepo wako unaobadilisha na kukaribisha kile ambacho ni kipya kwetu, leo na kila siku.

### Wimbi la Maombi

**Januari 22-24** Misri; Gasabo -Rwanda; Otukpo & On the Coast - Nijeria; Bathurst - Australia na Nasik in India

**Januari 26-28:** False Bay –Afrika Kusini; Shinyanga - Tanzania; Umuahia & Ijebu South West-Nijeria; Bath & Wells – Uingereza na Vellore- India

**Januari 29-31:** Masvingo -Zimbabwe; Kibondo - Tanzania; Nebbi - Uganda; Bida - Nijeria; Llandaff -Wales na Kanyakumari - India

**Jumapili 30**
Sifa Zote kwa Mungu akitutegemeza, akitukomboa na kutubadilisha, shukrani Milele. Tusifu Utatu tunaoupenda. Kitabu cha Maombi cha New Zelandi

**Jumatatu 31**
Bwana mwenye Upendo, badilisha maisha yetu ili tuweze kuangazia utukufu wa Kristo. Endelea ndani yetu kazi ya Roho wako; muujiza wa mabadiliko ili kuakisi utukufu wa Kristo na kushiriki upendo wake ulimwenguni. Amina

**Ola de oración**

**Januari 29-31:** Masvingo-Zimbabwe; Kibondo - Tanzania; Nebbi - Uganda; Bida - Nijeria; Llandaff -Wales na Kanyakumari –India

## Kuondoa Umaskini nchini Burundi

IMANI KWA VITENDO

**... ikiwa unajitolea kwa ajili ya wenye njaa na kutosheleza mahitaji ya wanyonge, basi nuru yako itang'aa gizani, na usiku wako utakuwa kama adhuhuri.**

*Isaya 58:10 (NIV)*

MU nchini Burundi inapanga kuanzisha mradi mwendelevu wa Kusoma na Kuandika, na Uwezeshaji wa Jamii Kiuchumi. Hii italenga usaidizi kwa wanawake ambao ni watoa huduma pekee kwa ajili yao wenyewe na familia zao, ili kufungua uwezekano wao wa kiuchumi na kijamii kupitia uwekaji akiba shirikishi wa kusoma na kuandika na duru za mafunzo ya biashara.

Kazi hii ikifanyika katika Dayosisi za Buhiga, Rutana & Mutana, na kwa ushirikiano wa karibu wa MU na kanisa, washiriki watakuwa na nafasi ya kujiondoa kutoka kwa umaskini.

Tunalenga kutambua na kutoa mafunzo kwa Wawezeshaji wa Hiari (VFs) ili wafanye kazi ndani ya jumuiya zao katika Dayosisi zote, kila mmoja akiunda kikundi cha mafunzo kwa wanawake wenyeji. Washiriki watapokea elimu kwa njia hii kwa muda wa miaka miwili na kutiwa moyo kuchukua nyadhifa za uongozi ndani ya jumuiya na makanisa yao. Wanapojiamini katika kujua kusoma na kuandika, washiriki watahimizwa kuhudhuria vikundi vya MU vya kuweka akiba. Watajifunza kutambua fursa za biashara na kukuza ubia uliopo.

**Ombea:** wanawake ambao ni watoa huduma pekee, ili tuweze kusaidia kufungua safu mpya za uwezekano kwao.